* HABARI LEO UK 4. *

# Bil 110/- zatengwa kuendeleza uvuvi

**Na Nashon Kennedy, Mwanza**

SERIKALI imetenga Sh bilioni 110 kuendeleza sekta ya uvuvi katika maeneo tofauti ikiwa ni pamoja na kununua boti za uvuvi na injini zake.

Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega alisema jijini Mwanza kuwa lengo la utoaji wa fedha hizo ni kuwezesha nchi kuendelea kunufaika na rasilimali za uvuvi.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi, utekelezaji wa mipango mikakati ya kitaifa, kikanda, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano (2021/22-2025/26) na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2020-2025) kupitia ibara yake ya 18(a)(v) 27(c) na Ibara ya 43(a) hadi(q).

Ulega alisema kupitia ibara hizo, serikali imesisitiza umuhimu wa ujenzi na ukuaji wa uchumi wa kisasa, shirikishi na shindani kupitia viwanda utakaowezesha ustawi wa jamii na kuongeza mchango wa rasilimali za maji na kutengeneza fursa za ajira na kupunguza umaskini wa kipato.

Aliitaja miradi mingine ambayo fedha zimetengwa ni pamoja na ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ujenzi wa mialo mitatu na masoko saba, mitambo ya kuzalisha barafu na vichanja vya kukaushia dagaa lengo likiwa ni kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na kuongeza thamani na masoko ya mazao ya uvuvi.

Alisema kati ya fedha hizo zilizotengwa, Sh bilioni 50 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ambao umeanza katika eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi.

Kwa mujibu wa waziri, sekta ya uvuvi inatoa ajira milioni 4.5 kwa Watanzania kwenye mnyororo mzima wa thamani zikiwamo ajira za wachakataji wa mazao ya uvuvi, wafanyabiashara, watengenezaji wa zana za uvuvi, wakuzaji viumbe maji, wachuuzi, mama na babalishe.

---

ipa
uhi

lo ana majonzi
wa na binti yake
ikuwa na watoto
a yupo mmoja
nepatwa na
kudumu baada
shituko," alidai

nde wa mdai
shukuru ma-
kutenda haki
uwa katika kesi
amoyo.
naendelea
na kitendo cha
basi hilo kuto-
damu na uhai wa
abu tangu ajali
wakuwahi kuona
atika kampuni
mbani kwake au
kutoa pole na
jishughulisha
amna yoyote ile,
kama hakuna
kea," alisema

uwa walichoki-
kuondoa gari lao
isi na kuendelea

olea
0,000

i, mawasiliano
umeme ili
o kiendelee na

ka Watanzania
azi kiwan-
va waaminifu,
kwa weledi na
zi wazuri kwa
engine wataka-
za nchini.
Kilimo, Hussein
ka mawakala
mbolea ya ru-
kazi hiyo kwa
kuwa serikali
tawachukulia
takaobainika
anyifu.
i mkuu wa
, Nduwimana
a ujenzi wa
ulianza Julai
aza uzalishaji
na kuajiri

a laini ya pili
hafika na ujen-
a mwakani
kamilisha
nbo itakayo-
ioni moja kwa
a.
ema wa-
nazalisha
bora, viwango
i kwa udongo
eneo husika.